

Kiswahili kama Nyenzo ya Maendeleo Nchini Kenya

Mwenda Mukuthuria

Ikisiri

Ukuzaaji na uendelezaji wa Kiswahili kama lugha ya taifa nchini Kenya ni lengo la taifa ambalo bado halijapewa kipaumbele kinachostahili. Hata hivyo, tangu Kenya ilipojinyakulia uhuru, matumizi ya lugha hii yamepevuka kinyume na matarajio ya wengi, kiasi kwamba, kwa sasa, mchango wake katika kufanikisha maendeleo ya sehemu za mashambani¹ hauwezi kukadiriwa. Nia ya makala haya ni kubainisha mchango huu katika kufanikisha malengo ya kitaifa katika sehemu za mashambani. Ili kufanikisha lengo la makala haya, kielelezo cha nadharia ya mawasiliano kinachotilia maanani hali halisi ya sehemu za mashambani Kenya kitatumika. Lengo kuu ni kuthibitisha jinsi ambavyo mikakati ya kukuza Kiswahili, kama lugha ya kutegemewa katika nyanja zote, haiwezi kutepukika hasa katika kipindi hiki ambacho jitihada za kuunda Jumuuya ya Afrika Mashariki zimeshika kasi. Mwisho makala yameainisha vikwazo vinavyokikumba Kiswahili katika maeneo haya ya mashambani pamoja na kutoa mapendekezo ya kudhibiti na kuimarisha lugha hii kama nyenzo ya maendeleo sehemu za mashambani na katika taifa la Kenya kwa ujumla.

1.0 Utangulizi

Kila shughuli ya mwanadamu inategemea mawasiliano ya lugha ambayo yana manufaa zaidi kuliko aina nyingine yoyote ile ya mawasiliano. Kwa hivyo, kimsingi, lugha ndiyo nguzo kuu ya kuunganisha jamii-lugha na kufanikisha kila hatua ya maisha. Pamoja na umuhimu huu, nchi nyingi zilizokuwa chini ya tawala za kikoloni hazitili maanani umuhimu wa lugha za asili. Ni kutokana na sababu hii nchi nyingi za Kiafrika baada ya kujinyakulia uhuru ziliendelea kutumia lugha za kikoloni. Kwa kufanya hivi, uzembe wa kutoendeleza lugha za wenyiji ulianza kukita mizizi na mpaka karne ya 21 hali hiyo hajarekebishwa katika nchi nyingi mfano Kenya, Uganda, Malawi, Sudani na Kongo. Hata pale ambapo lugha fulani imeteuliwa kuwa lugha ya taifa, kwa mfano Kiswahili nchini Kenya, ni wazi kwamba serikali haina sera mwafaka ya kukuza lugha hii ili iweze kukabiliana na mabadiliko ya kiutandawazi ambayo yana nafasi kubwa katika ulimwengu wa kisasa. Matokeo ya hali hii ni kwamba lugha za asili zimetengwa na kunyimwa fursa muhimu ya kuchangia katika maendeleo ya taifa. Kwa mantiki hii, makala yanaweka wazi mchango wa lugha ya Kiswahili kama nyenzo ya maendeleo katika sehemu za mashambani nchini Kenya. Makala yatatalii jinsi lugha hii ilivyofanikisha malengo ya kitaifa katika sehemu za mashambani. Ili kuthibitisha uwezo wake kimawasiliano, dhima za lugha hii zitachunguzwa kwa misingi ya nadharia ya

¹ Istilahi hii inatumika nchini Kenya ikiwa na maana ya vijijini kwa Tanzania.

mawasiliano. Vilevile, makala haya yataangazia mikakati ya kukuza Kiswahili kama lugha ya kutegemewa, vikwazo vinavyokumba Kiswahili katika maeneo haya na hatimaye yatatoa mapendekezo ya kudhibiti na kuimarisha lugha hii adhimu.

2.0 Lugha na Maendeleo

Lugha ni nyenzo ya kufanikisha maendeleo. Nyenzo ni zana au kifaa cha kuwezesha utekelezaji wa kazi fulani. Maendeleo ni mabadiliko chanya katika jamii ambayo hutokana na mipango madhubuti. Maendeleo yanapaswa yaangaliwe kama ukuaji na mabadiliko chanya katika nyanja mbalimbali za maisha ya binadamu. Kwa mujibu wa Todaro (1994), maendeleo ni mchakato changamani unaoshirikisha mabadiliko ya mfumo-jamii, mielekeo pendwa, asasi za kitaifa pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi, upunguzaji wa hali ya kutokuwa na usawa na uangamizaji wa umaskini. Maendeleo kimsingi yana lengo la kufanikisha wananchi kujifunza teknolojia mpya, kuimarisha hali zao za maisha kwa kutumia teknolojia hiyo, kuwapa habari za kuepukana na maradhi, kuwaimarisha kibiashara, kuendeleza amani na kuwafahamisha sera za serikali. Katika maendeleo lugha ina manufaa yafuatayo:

Kwanza katika maeneo ya mashambani, lugha ni chombo muhimu sana katika kuelezea mambo ya msingi kama vile shughuli za kilimo, za afya na nyinginezo. Hii husaidia kukuza uelewa wa jamii na hatimaye kufanikisha shughuli za maendeleo.

Pili, kupitia lugha, jamii huweza kusikia maelezo na kuyahifadhi akilini kwa kutumia lugha iliyotumiwa kuyawasilisha maelezo yanayohusika, au wakati mwingine kufasiriwa kwa lugha nyingine. Aidha, kupitia kusoma vitabu na majarida jamii huweza kuelewa jambo au matukio fulani. Bila shaka majarida na vitabu huandikwa kwa lugha mahususi. Mwanadamu anaona na kusikia kisha anatumia lugha kueleza yale aliyoyaona na kuyasikia. Lugha ni chombo pia cha kufundishia na kujifunzia maarifa mbalimbali yanayoweza kuiletea jamii au mtu binafsi maendeleo. Kwa ujumla, kuna uhusiano mkubwa kati ya maendeleo na lugha.

3.0 Nadharia ya Mawasiliano

Nadharia hii iliasisiwa na Claude Shannon na Warren Weaver mwaka 1949 (Severin na Tankard, 1992). Msingi mkuu wa nadharia ya mawasiliano ni kwamba lugha ni mfumo wa kimawasiliano. Nadharia hii inasisitiza kwamba, kila ujumbe una *chanzo*. Vipengele vingine ambavyo vinatiliwa maanani katika nadharia hii ni kama vile *kienezi*, *kinachoeneza* ujumbe, *mfumoenezaji* (mbinu) unaotumika kueneza ujumbe, *kipokezi* ama mpokeaji wa ujumbe, na *kiishio*,

kilichokusudiwa ujumbe. Kipengele cha kelele kilichangiwa na Wiener (1948) ikiwa na maana ya mambo au hali ambayo inaweza kukwamisha mawasiliano. Kwa mfano, katika hali ambapo watu wanatumia lugha zisizo na uelewano, tofauti hii ya mifumo ya lugha ni kikwazo ambacho kinaweza kuzorotesha mawasiliano. Aidha, Wiener aliongeza pia kipengele cha *matokeo* katika mawasiliano.

Ili kuhakikisha kwamba mawasiliano hayakwami Shannon na Weaver walionelea kwamba lazima kuwe na hali ya *entropi* na *uradidi*. Entropi na uradidi ni hali mbili ambazo zinapaswa kuwekwa katika mizani sawa ili kuimarisha mawasiliano. Usawa wa hali hizi huleta kutabirika na kutotabirika kwa ujumbe. Chanzo cha ujumbe wa lugha ni ubongo wa watumizi wake, na ujumbe ambaa unaleta athari ni mazungumzo, maneno yaliyoandikwa au muziki.

Kwa mujibu wa nadharia hii, kienezi ni kama mfumo-sauti ambaa hutoa sauti zinazotumika katika mawasiliano ya lugha. Watu wanapozungumza, hewa ndiyo mfumo-enezi wa ujumbe. Kama ni maandishi, karatasi hufanya kazi hii. Kulingana na Weaver, mfumo-enezi una kiwango cha ujumbe ambaa unaweza kueneza. Kiwango hiki kinategemea wakati na muda. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuendeleza lugha ili iweze kukabiliana na masuala ibuka ya kiteknolojia ili kufanikisha upitishaji wa maarifa mapya kwa ajili ya kujenga daraja baina ya wataalamu na watumiaji wa maarifa.

Ili kuthibitisha kuwa mawasiliano yamekamilika, matokeo ndiyo kiainisho muhimu. Kila ujumbe unaowasilishwa kwa ajili ya kuleta mabadiliko, unapopokelewa na kutekelezwa, huashiria kwamba mawasiliano yamekamilika.

Dhana ya mawasiliano ina upana wake kimatumizi na inaweza kutumiwa kutanzua uhusiano wa kila aina katika mifumo na matokeo yake. Ingawa ujumbe kwa mujibu wa nadharia hii hauwezi kutabirika, ni muhali kutaja kwamba ujumbe wa lugha ulio na ufasaha na unaowafikia walengwa na matokeo yake vinaweza kutabiriwa. Ukweli huu una mashiko tukizingatia kwamba nadharia hii inashikilia kuwa, ujumbe ukiwa umepangiliwa barabara, hali ya kutotabirika inapungua.

3.1 Nadharia ya Mawasiliano na Utendakazi wa Lugha

Kwa mujibu wa Nadharia ya Mawasiliano, mawasiliano yoyote ya mwanadamu huwa na chanzo chake (Rono, 2001). Kimsingi, lugha ni mfumo wa ishara ambaa hutumiwa na wanadamu kwa ajili ya mawasiliano. Hii ina maana kwamba jukumu la lugha ni kufanikisha mawasiliano. Ili mawasiliano ya lugha

yakamilike, ishara za lugha lazima zieleweke kwa mpokeaji wa ujumbe. Aidha, chanzo chake kisiwe na kikwacho cha aina yoyote ili ufasiri wa ujumbe uwe rahisi kwa mpokeaji. Kwa hiyo, iwapo jamii-lugha inatumia mfumo mmoja wa lugha kwa ajili ya mawasiliano, ina maana kwamba mawasiliano baina ya jamii-lugha husika hayana vikwazo. Katika mazingira ya Kenya ambapo pana jamii ya wingi-lugha, nafuu ya mawasiliano hupatikana kwa matumizi ya Kiswahili ambacho kinaelewka na watu wengi. Kuelewka kwa lugha hii na watu wengi kunatokana na ukweli kwamba Kiswahili ni lugha iliyio na asili ya Kibantu. Hivyo, Wakenya wengi walio na asili ya Kibantu huielewa barabara. Ufanisi wa lugha hii kimawasiliano pia umetokana na maamuzi ya serikali ya kuiteua kuwa lugha ya Taifa. Hali hii imefanya lugha hii kupokelewa na takriban Wakenya wote. Hii ndio sababu nchi ya Kenya iliamua kuifanya lugha hii kuwa rasmi kikatiba mwaka 2010. Kwa hiyo, Kiswahili ndiyo lugha ya pekee inayoweza kutumiwa katika mawasiliano mapana.

Nadharia ya mawasiliano inatilia maanani mambo yafuatayo: chanzo ama asili ya ujumbe, mpokeaji wa ujumbe na athari za ujumbe. Chanzo kinaweza kuwa mtu mmoja, au kikundi cha watu. Katika nadharia hii pia, mfumo ni mbinu ambayo inateuliwa na chanzo cha ujumbe kumfikishia mpokeaji ujumbe. Mpokeaji wa ujumbe ni mhusika anayetazamiwa kupata athari kutokana na ujumbe na athari ni mabadiliko hasi au chanya yanayopatikana kwa mpokeaji kutokana na ujumbe fulani. Upokeaji wa ujumbe unakuwa chanya au hasi kutegemeana na utamaduni, mielekeo na maarifa aliyonayo mpokeaji, na kadhalika. Mfumo wa kuwasilisha ujumbe sharti uwe sahili. Mfumo unaweza kuwa ishara za lugha ya maandishi, maneno ya mdomoni, ishara za mwili zisizo na misingi yake katika lugha, nyimbo, na kadhalika.

Ukamilifu wa mawasiliano yoyote yale unatokea pale ambapo athari za ujumbe zinawasilishwa kwa chanzo kwa ajili ya kupokelewa na kufasiriwa ili kung'amuwa iwapo uelewano umetokea. Ni kutokana na hali hii ndipo maamuzi ya mawasiliano chanya yanaweza kufikiwa.

4.0 Kiswahili kama Nyenzo ya Maendeleo nchini Kenya

Katika mazingira ya Kenya, Kiswahili ndiyo lugha pekee inayokidhi kuwa mfumo wa mawasiliano ya aina yoyote ile yanayohusisha lugha. Kwa mfano, Kiswahili ni lugha yenye asili ya Kibantu na hivyo, inaelewka na watu wengi ambao wanatumia lugha za Kibantu katika mazingira ya Kenya kama vile Waluyia, Wakikuyu, Wakamba, Wameru, Waembu na Wamijikenda. Vilevile, utamaduni wa lugha hii ni wa asili ya Kiafrika. Kwa hivyo, inaweza kufanikisha uwasilishaji wa maarifa na teknolojia ya asili, jambo ambalo limepuuzwa kwa miaka mingi kwa kupendelea teknolojia ya kigeni. Kwa

mfano, tiba za kiasili zinaweza kuelezewa kwa urahisi kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu mimea inayotumika inapatikana katika mazingira ya Kenya na inaeleweka na jamii mbalimbali zinazozungumza Kiswahili.

Hali kadhalika, lugha hii inaeleweka na watu wengi ambao wanatumia lugha zao za asili za Kibantu zilizo na uelewano sambamba na Kiswahili. Kwa hivyo, haina vikwazo vingi vya kiutamaduni ikilinganishwa na lugha za kimagharibi kama vile Kiingereza na zingine. Hii ni kwa sababu utamaduni wa Kiswahili umeenea Kenya. Kutokana na hali hii lugha hii inafaa sana katika kupitisha ujumbe unaohusu maendeleo yanayomhusisha Mkenya. Kwa jinsi hii, inawafanya wananchi kujiamini na kupata uwezo wa kutekeleza shughuli zao (Mohamedin, 2001).

Mazingira mengine yaliyoipa lugha hii nafasi ya kutumika kama nyenzo ya maendeleo ni kwamba ilipopitishwa kama lugha ya taifa mwaka 1974 ilipanua matumizi yake kwa watu wengi. Jambo hili lilifanya lugha hii kuwa ya utawala na kupanua matumizi yake kwa watu wengi. Hivi leo, ndiyo lugha inayotumiwa na machifu, maafisa tawala, wakuu wa wilaya na watawala wengine kuwasilisha sera za serikali. Aidha, wataalamu wa nyanja mbalimbali wanatumia lugha hii kuwaelimisha wananchi kuhusiana na masuala ya kimaendeleo. Katika mfumo wa elimu, lugha hii imepewa kipaumbele kama somo la lazima; na hivyo, idadi ya watumiaji wa lugha hii imepanuka na kuongezeka tangu kuanzishwa kwa mfumo wa 8-4-4 mwaka 1985. Pamoja na dhima hizi za lugha ya Kiswahili, lugha hii imekubaliwa kama lugha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hivyo, ni lugha iliyo na ushawishi kwa Wakenya wengi ili waweze kuitumia kwa mapana katika kanda hii ya Afrika Mashariki.

Uwezo mwagine wa lugha hii ni kwamba inawafikia Wakenya bila kuwabagua kwa misingi ya elimu (Mutahi, 2001). Inafaa pia kufundishia na kuelimisha makundi lengwa kwa urahisi. Kwa jinsi hii, teknolojia inaweza kupitishwa kwa urahisi na mapendekezo ya wataalamu yanaweza kueleweka kwa urahisi. Jambo hili linawasaidia wataalamu kupendwa na kuaminiwa na wananchi, jambo ambalo linarahisisha utendaji wao. Katika mwelekeo huu inawasaidia pia wahudumu wa umma kuwafikia Wakenya wasio na uwezo wa kuwasiliana kwa Kiingereza. Hii inasaidia kuongeza uzalishaji katika nyanja mbalimbali za maendeleo wanazozishiriki, na hivyo kuboredsha hali zao za maisha.

Mnano mwaka wa 2010, Kiswahili kilipata hadhi ya kuwa lugha rasmi ya pili kikatiba nchini Kenya. Jambo hili lilifanya lugha hii kupendwa na wananchi wa Kenya. Awali kulikuwa na wasiwasi kutokana na lugha ya Kiingereza

kuchukuliwa kama lugha ya hadhi ya juu kwa kuwa imetumika kama lugha rasmi tangu uhuru. Hivi leo, Kiswahili ni lugha adhimu na wakulima hawaoni aibu wanapoitumia ama kusoma maandishi ya lugha hii.

4.1 Mchango wa Kiswahili katika Maendeleo Nchini Kenya

Swali muhimu la kuijiliza hapa ni: Je, ni maendeleo yapi yanaweza kuchangisha na Kiswahili? Katika kujibu swali hili ni vyema kudokeza kwamba lugha inachangia takriban nyanja zote kwa vile bila mawasiliano ya lugha, hakuna maendeleo. Nyerere (1967) na Todaro (1980) wanaafikiana kwamba lugha inaweza kuchangia nyanja za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa mfano, lugha inatarajiwa kuimarisha hali ya maisha ya jamii. Hii ni pamoja na kuimarisha kasi na kiwango cha huduma za jamii. Huduma hizi ni kama vile elimu, afya, maji, na zinginezo. Iteleweke kwamba uimarishaji wa viwango vya huduma katika jamii hauwezi kutekelezwa bila watu kufahamu yale yanayopaswa kufanyika. Lugha ya kufanya hivi katika mazingira ya Kenya si nyingine ila ni Kiswahili. Lugha hii itatekeleza jukumu hili pale inapozingatiwa kama lugha inayoeleweka na ambayo msamiati wake unaafikiana na utamaduni, mazingira na kile kinachozungumzwa kwa ujumla.

Kiswahili nchini Kenya hutumika kuhamasisha watu kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Kuongezeka kwa watu na viwanda katika mazingira ni jambo ambalo linawaleta Wakenya dhiki kubwa. Njia pekee ya kulitatua tatizo hili ni kuwafikia wananchi na kuwaelimisha jinsi ya kukabiliana na tatizo hili. Tangu uhuru ulipopatikana Kenya mwaka 1963, viongozi wa nchi wamekuwa wakiwahamasisha wananchi kukabiliana na janga hili kwa kutumia Kiswahili kutokana na jamii hii kuwa na lugha nyingi. Imewezekana kutekeleza jukumu hili kwa vile Kiswahili ni lugha ya taifa na imeenea sana kuliko lugha za wenyiji. Jambo hili limewezekana kwa sababu ujumbe umeweza kuwafikia Wakenya wengi kupitia mabango yaliyoandikwa kwa Kiswahili; vyombo vya habari kama vile redio na runinga; hotuba za viongozi kama vile wakuu wa wilaya/ maafisa tawala, na machifu.

Iwapo maendeleo yoyote yataweza kufikiwa, wananchi hawanabudi kujua haki zao; hivyo, hili ni jukumu lingine la kuchochea maendeleo linalotekeliza kupitia Kiswahili katika mazingira ya Kenya. Kiswahili ni lugha ambayo imetumika kuwafelimisha Wakenya kuhusu haki zao za kiraia kama vile uchaguzi wa viongozi, haki za waajiriwa, za kisheria, biashara, ukulima, za dini na nyingine nyingi. Kimsingi, iwapo raia hawajui haki zao katika jamii, dhuluma inaweza kuendelezwa dhidi yao kila mara. Katika mazingira ya Kenya, Kiswahili hutumika kufafanua haki za kila aina ili zieleweke kwa watu wote kwa vile ndiyo mfumo ufaao wa mawasiliano. Kwa mfano, Katiba mpya ya

mwaka 2010 imeandikwa kwa Kiswahili ili ipate kueleweka kwa Wakenya wa matabaka yote. Ikifanyika hivi, ujumbe muhimu unakuwa umeepuka kikwazo cha mawasiliano cha kutafsiri (kelele) ambacho kinaweza kupotosha ujumbe. Vilevile, *iktisadi* ya kuendeleza harakati hizi inapatikana kwa kuepuka matumizi ya lugha nyingi ambazo zinaweza kuwa si kikwazo pekee bali ni gharama kubwa ya kuendesha shughuli nzima ya mawasiliano.

Lugha ya Kiswahili pia, imechangia maendeleo katika mfumo wa elimu kwa kutumika kama nyenzo ya kuwafundisha watoto katika maeneo ya miji ya Kenya na sehemu nyingine ambazo watu wa jamii mbalimbali wanaishi. Kwa jinsi hii, inasaidia kufanikisha ujifunzaji wa maarifa. Akizungumzia lugha ya ufundishaji, Dutcher (1982) anadai kuwa lugha inaweza kuwa kikwazo au kiamuzi cha matokeo ya wanafunzi katika viwango vya shule ya msingi na shule za upili. Mwandishi huyu anaendelea kusisitiza kwamba hali kama hii inaweza kuamua iwapo mwanafunzi ataendelea na elimu katika viwango vya juu au la. Maoni haya yana ukweli ambao unaweza kuwachangamsha wataalamu wa elimu popote pale. Fasili yake ya kimawasiliano ni kwamba ujifunzaji wa maarifa hutegemea lugha kwa kiwango kikubwa sana. Hii ina maana kwamba lugha inayotumiwa na mwanafunzi lazima iwe inaendana na tajriba zake za maisha ili iweze kufanikisha ujifunzaji wa maarifa.

Tatizo kubwa la nchi kama Kenya ni kwamba ina lugha nyingi za kiasili na lugha hizi zote haziwezi kutumiwa katika mfumo wa elimu. Changamoto hii inaashiria kuwa katika maeneo ya mashambani ya Kenya, ambako watoto hujifunza lugha za kienyeji kama lugha za kwanza, wanalazimika kujifunza lugha mbili zaidi – Kiingereza na Kiswahili. Kwa mujibu wa nadharia ya mawasiliano, kwa kiwango kikubwa, jitihada za kujifunza lugha nyingi zina athari zake. Kwanza, anayejifunza, hatafikia umilisi wa kileleni katika lugha zote. Hii ni kwa sababu, kwa kila lugha anayojifunza ataathiriwa na lugha ya kwanza kimuundo na kimitindo. Ukweli unaobainika katika mazingira ya Kenya baada ya watoto kujifunza Kiingereza na Kiswahili ni kuwa Kiingereza huishia kutumika shulen, lakini watoto huendelea kutumia Kiswahili hata wanapotoka shulen. Kwa jinsi hii, wanafunzi wengi wa shule za mashambani huishia kuwa na umilisi wa hali ya juu wa Kiswahili kuliko Kiingereza. Hali hii ina faida kwa upande wa mawasiliano mapana. Hata hivyo, kwa upande mwingine, hasa katika kujifunza shulen ambapo Kiingereza hutumika kama lugha ya kutahini mitihani yote, inaashiria kwamba wanafunzi watakuwa na upungufu katika kujieleza. Athari yake ni kwamba kutakuwa na matokeo duni. Hali hii inadhihirika sana wakati matokeo ya shule zinazosisitiza matumizi ya Kiingereza yanapolinganishwa na ya shule ambazo hazina mwelekeo huu (Mohochi, 2005). Tatizo hili lina misingi yake katika kutumia lugha ya

Kiingereza kutahini mitihani yote, badala ya Kiswahili. Kwa hivyo, ikiwa wanafunzi wa mashambani wanashindwa kufaulu mitihani ambayo ni kipimo cha upataji wa maarifa, bila shaka huku ni kurudi nyuma kimaendeleo kwa kuwa malengo ya elimu ya kitaifa hayatafanikiwa. Ifahamike kwamba nchi yoyote ambayo malengo yake hayatimii haiwezi kuona maendeleo ya haraka. Nchi zote ambazo zimepiga hatua kubwa kimaendeleo kama vile nchi ya Korea, Japani na Uchina nguzo muhimu iliyofanikisha maendeleo hayo ilikuwa ni matumizi ya lugha zao za asili.

Nyanja nyingine ambayo imefanikiwa kupitia Kiswahili ni siasa. Siasa ni hali ya maisha kwa ujumla, hasa uwezo na mamlaka katika maisha ya kawaida. Mkabala wa utumiaji wa uwezo na mamlaka ndio unaojenga itikadi, mkondo wa falsafa ambayo busara yake inaweza kutumiwa kuelekeza jamii katika kipindi fulani cha historia. Ni muhali kutaja kwamba kila itikadi ya kisiasa huhitaji lugha kama nyenzo iwapo itaeleweka kwa watu wengi. Ni katika kifundo hiki ambapo lugha na siasa zinakutana. Wazo hili linadhihirika wazi wakati ambapo kuna kampeni maeneo ya mashambani. Katika kuzungumzia ruwaza zao, taarifa za wanasiasa kuhusiana na sababu za kupata mamlaka, kuyagawa na kuongoza nchi hupitishwa kutoka eneo moja hadi lingine kupitia nyimbo za Kiswahili. Kwa mfano, nchini Kenya uchaguzi wa kuamua iwapo katiba mpya iliyokuwa ikiundwa ipitishwe au isipitishwe mwaka wa 2006 ulitumia ishara ya maneno mawili – *ndizi na chungwa*. Aidha, lugha iliyotumiwa kuwazindua na kuwashamasisha wananchi wa Kenya ilikuwa Kiswahili. Ilivyobainika kipindi hiki ni kwamba Kiswahili kina nafasi ya uhamasishaji wa umma isiyo na kifani. Hali hii ilitokea kuwa hivyo kwa sababu wanasiasa walikuwa wakijitakia ufanisi kisiasa.

Hata hivyo, ni muhali kutaja kwamba uwezo wa lugha hii ya Kiswahili hauonekani pale ambapo wanasiasa hawajitakii ufanisi wa siasa za kitaifa. Kwa hivyo, kimsingi wanadunisha Kiswahili bungeni wakati maamuzi yao yanahitajika ili kufanikisha lugha hii kusonga mbele. Lau wangejua kwamba uwezo wa lugha hii hauna kifani katika kuyaendeleza masuala yanayoathiri taifa hili kwa ufanisi kama vile inavyowawezesha kufanikiwa kisiasa, wasingejwekeva vikwazo kama kuidhalilisha katika mfumo wa elimu ama shughuli yoyote ya kitaifa. Ifahamike kuwa ni lugha hii ya Kiswahili ambayo imefanikisha jitihada za serikali za kupambana na ujinga, kuwashamasisha umma kuhusiana na maradhi ya utapia mlo, UKIMWI, malaria na maradhi mengine. Kwa hivyo, ufanisi wa lugha hii katika kuyatekeleza majukumu hayo ni ithibati ya nafasi ya Kiswahili katika maeneo ya mashambani.

Aidha, katika bunge la Kenya, lugha hii imekubaliwa kutumiwa kuuliza maswali na kuendeleza mijadala. Tatizo linalokumba Kiswahili kwa sasa katika kufanikisha jambo hili ni kwamba kumbukumbu za mijadala haziandikwi kwa Kiswahili ila zinahifadhiwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, ni muhimu lugha ya Kiswahili itumike katika kuhifadhi kumbukumbu za mijadala ili yanayojiri bungeni yaweze kuwafikia Wakenya wa kawaida katika uasilia wake. Kwa jinsi hii, watapata nafasi ya kujuu mkondo unaochukuliwa na uongozi wa taifa. Vilevile, kitendo hiki kitathibitisha kwamba maamuzi yao ya kufanya Kiswahili kuwa lugha rasmi hayakuwa ya kinadharia tu bali pia ya kivitendo.

Mchango wa Kiswahili pia unaweza kuonekana katika masuala ya maendeleo ya uchumi nchini Kenya. Suala la uchumi ni pana mno. Linahusu uzalishaji mali, usambazaji bidhaa na utoaji huduma ili kutosheleza mahitaji ya kijamii (Todaro, 1985). Katika hali hii ya kutosheleza mahitaji, lazima mtu aone ni mali ipi inayohitaji kuzalishwa, itazalishwa kwa kiasi gani na itasambazwa kwa namna gani. Ifahamike kwamba mtu hawesi kuzalisha ama kusambaza bidhaa asiyoijua. Kwa hivyo, ni lazima lugha itumiwe kuelezea mchakato mzima wa uzalishaji wa bidhaa, usambazaji na huduma zinazohitajika. Iwapo haya yote yatafanikiwa, lugha inayoelewaka na kutumika na wengi ni sharti itumike. Akizungumzia umuhimu wa lugha katika uchumi hasa katika eneo la Mumias nchini Kenya, Amenya (2007) amedai kwamba uuzaji wa hisa za kampuni ya Mumias ni suala ambalo halikuelewaka kwa wakulima kwa sababu ya matumizi ya istilahi ya Kiingereza *shares* ambayo hawakuweza kuifafanua wala kuielewa kwa Kiluhya. Hivyo, wengi wa waliogawiwa hisa hizi walishawishika kuziuza hisa zao kwa bei duni bila kutilia maanani faida ambayo wangepata iwapo wangezihifadhi kama kitega uchumi. Maoni ya mwanazuoni huyu ni kwamba, dhana ya hisa haikuwasilishwa kwa wakulima kwa lugha ambayo wangeielewa vyema. Kwa jinsi hiyo, matapeli waliwavamia wakulima na kuafilisi hisa, jambo ambalo lisingetokea iwapo uongozi wa kampuni ya Mumias ungewaelimisha wakulima kuhusiana na suala la hisa na umuhimu wake katika maendeleo ya kiuchumi kwa kutumia lugha inayoelewaka kwa wakulima. Kwa hiyo, mfano huo wa Amenya (2007) ni kielelezoo bora cha jinsi lugha isiyoelewaka kwa watu inavyoweza kusababisha dhuluma katika jamii na kuzorotesha uchumi. Kimsingi, utumiaji wa bidhaa za viwandani, ufanikishaji wa maendeleo ya mbinu za kilimo, biashara ya juakali² na biashara zingine ndogondogo katika maeneo ya mashambani nchini Kenya zinategemea lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kuwepo kwa jamii zinazozungumza lugha tofauti.

² Biashara ya Juakali ni biashara ya viwanda vidogo vinavyoinukia ambapo bidhaa hutengenzwa na kuuzwa kwa rejareja.

Maeneo mengine ya kiuchumi ambayo yanatokana na Kiswahili ni pale ambapo watu walio na ujuzi wa lugha hii wanatumia kujipatia ajira kama walimu au wafasiri na kupata mapato yanayoimarisha hali zao za maisha. Aidha, watu walio na elimu wanatumia Kiswahili katika kufanikisha mikataba inayoeleweka kwa wafanyabiashara ili kukuza shughuli za kuuza na kununua bidhaa, kuandika kumbukumbu za mikutano ya vikundi vya maendeleo, kuandika mikataba ya kukodisha mashamba na kadhalika.

Katika nyanja ya teknolojia pia, Kiswahili kina mchango wake. Teknolojia inahusu utumiaji wa maarifa, ujuzi ama vifaa vya kisayansi kurahisisha kazi za binadamu anapokuwa katika harakati zake za kupambana na maisha ya kila siku. Dhana ya teknolojia haijawasilishwa ipasavyo katika maeneo ya mashambani nchini Kenya. Inavyoeleweka ni kwamba sayansi na teknolojia ni maarifa ya kutoka katika nchi za Magharibi. Kuna uvumbuzi mbalimbali katika sehemu za mashambani. Hata hivyo, matumizi ya uvumbuzi huo kurahisisha utendaji wa Wakenya kwa ujumla hayajafanikiwa kwa sababu teknolojia inayohusika inaeleweka kwa lugha finyu za kienyeji na kutumika katika eneo finyu pia. Akizungumzia hali hii Amenya (2007) anatoa mfano kwamba vikapu vya kuhifadhi joto la chakula vijulikanavyo kwa Kiingereza kama *fireless cooker* (jiko lisilo na moto) vimekuwepo Kenya kwa muda mrefu. Aidha, meko ya kutumia kuni inayohifadhi joto na kutumia kuni chache imekuwepo kwa muda mrefu mionganoni mwa jamii za Wakenya. Hata hivyo, watu wengi wa kutoka sehemu za mashambani nchini Kenya hawakuwa na habari ya kuwepo kwa vifaa hivi hadi Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC) lilipochunguza teknolojia hii na kuelezea nafuu inayopatikana kutokana na matumizi yake katika matangazo yaliyopeperushwa kwa Kiswahili. Mfano huu wa Amenya ni kielelezo cha jinsi ambavyo teknolojia rahisi ya kienyeji inaweza kurahisisha shughuli za watu za kila siku. Teknolojia hii inaweza kuenezwa kwa lugha inayoeleweka na kutumiwa na watu wengi. Kuna teknolojia nyingi za kiasili ambazo zinatokana na jamii zetu za Kiafrika lakini hazijulikani na zinatumia na watu wachache. Kwa hivyo, Kiswahili kina nafasi kubwa ya kusambaza teknolojia hizi ili ziwe na manufaa kwa Wakenya wote.

Ikichukuliwa kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Kenya, nafasi ya Kiswahili katika uwanja huu haiwezi kusahaulika. Kwa mujibu wa Hicks (1980) kilimo huimarika iwapo watu mashambani wataajiriwa moja kwa moja. Jambo hili hupunguza kiasi cha pesa kinachohitajika kuendeleza kilimo. Vilevile, hupunguza upoteaji wa mali na mapato. Ifahamike kwamba mawazo ya Hicks (1980) hayawezi kuwa na mashiko ikiwa watu wa mashambani watakuwa wakitumia nguvu bila maarifa. Ikizingatiwa kwamba idadi kubwa ya watu wanaoshiriki kilimo mashambani wana elimu ya kiwango cha chini, ni kweli

tukisema kwamba wanaelewa lugha mbili – lugha ya kwanza na Kiswahili. Kwa hivyo, ikichukuliwa kwamba maafisa wa kilimo si lazima watumie lugha ambazo zinatumwiwa na jamii za maeneo wanayoyahudumia, basi Kiswahili kinabakia kama lugha ya kuwaenezea wakulima hawa maarifa ya kilimo. Kwa mintarafu hii, maagizo ya upandaji, uzuiaji wa mmomonyoko wa udongo, uzuiaji wa kupe na maradhi ya mifugo hutolewa kwa wingi kwa kutumia Kiswahili. Jukumu hili linaloteklezwa na Kiswahili ni la msingi kabisa na bila shaka lina manufaa makubwa katika maendeleo ya taifa.

Akishadidia vikwazo vinavyowakumba wataalamu wa nyanja tofauti Mohamedin (2001) anasema kwamba, kwa sasa maarifa ya kisayansi yanawasilishwa ama kuelezweta kwa Kiingereza. Kutokana na hali hii, mtaalamu huyu anasema kwamba jambo hili ni kikwazo kikuu kinachokabili ujumbe unaotolewa na maafisa hao. Kikwazo kingine anachoeleza Mohamedin (2001) na ambacho anakipa kipaumbele, ni kile kinachohusu tafsiri inayopotosha; hasa tafsiri ya kutoka Kiingereza kwenda katika Kiswahili ama ya Kiingereza kwenda katika lugha za wenyeji. Hali hii inasababisha kutoleweka kwa teknolojia kwa urahisi. Kwa mfano, tafsiri ya maelekezo ya kutumia lugha ya Kiswahili katika simu ya *Nokia X2-01* yana upotoshaji kiasi kwamba mtumiaji wa simu hii anaweza kuamua kutumia lugha ya Kiingereza kuliko kutumia Kiswahili. Kwa mfano, *uju'be, ujum, uj'be, ujumbe* – hii ni mifano ya jinsi neno *ujumbe* linavyojitokeza katika simu hii. Udondoshaji wa sauti bila mfumo unatatiza hata wataalamu wa Kiswahili. Si mifano hii pekee, bali kuna mifano mingi inayovuruga lugha ya Kiswahili kiasi kwamba si rahisi kueleweka. Hali hii inasababishwa na makampuni yanayoongoza katika teknolojia kutumia matapeli kutafsiri habari pasipo kushirikiana na wataalamu wa taaluma hii. Kwa hivyo, hapana shaka kwamba iwapo wataalamu watachukua jukumu lao la ushirikishi, uchocheaji na uhimizaji wa maendeleo, basi hawanabudi kutumia lugha ya Kiswahili ambayo haitakuwa na upotoshaji kwa vile inaeleweka na wengi.

Ama kwa hakika, taifa haliwezi kupiga hatua zozote za kimaendeleo iwapo wananchi hawana afya. Katika mazingira ya Kenya, lugha ya Kiswahili ina mchango usio na kifani kuhusiana na suala la afya. Kama tulivyokwisha kusema hapo awali, wahudumu walioajiriwa na serikali kushughulikia masuala ya afya si lazima wawe wanafahamu lugha za jamii wanazozihudumia ingawa wanaweza kuwa wana uwezo huo. Hata hivyo, ifahamike kwamba kwa kiasi kikubwa maelezo hutolewa kwa Kiswahili kinachoeleweka kwa wengi. Hali hii imefanikisha juhudzi za serikali ya Kenya za kueneza habari za afya bora kwa umma, hasa zinazohusika na jitihada za kujikinga na maradhi kama vile

malaria, UKIMWI, ebola, mafua ya ndege, homa ya bonde la ufa, kichaa cha ng'ombe na maradhi mengine yanayohatarisha maisha ya Wakenya.

5.0 Mapendekezo

Kuna haja ya serikali ya Kenya kuwa na sera mwafaka ya ukuzaji wa Kiswahili, ili kiweze kukabiliana na maendeleo ya teknolojia. Jambo hili limepuuzwa siku nyingi. Ni vyema ifahamike kwamba umilisi wa lugha unawezesha mawasiliano yenye ufanisi kwa sababu mwasilianaji anaweza kujieleza kwa usafaha. Kwa jinsi hii anaweza kuhusiana na hadhira vizuri na kufanikisha mawasiliano yaliyo na tija katika maendeleo.

Ingawa kwa sasa Kiswahili kinatumika katika nyanja mbalimbali za maendeleo sehemu za mashambani, ufanisi mkubwa zaidi utapatikana ikiwa Kiswahili kitapewa uzito zaidi kuititia michezo ya kuigiza, hadithi na sarakasi zilizo na dhamira ya maendeleo. Mtindo huu unapendelewa sana na shirika la umoja wa mataifa linaloshughulika na masuala ya idadi ya watu katika kuhamasisha umma kupanga uzazi na kupunguza idadi ya watu. Iwapo mtindo huu utatumiwa na wataalamu wanaowahamasisha wananchi kuhusiana na masuala ya maendeleo, huku lugha ya Kiswahili ikitumiwa, bila shaka lugha hii itakuwa na nafasi kubwa ya kufanikisha maendeleo.

Kuna haja ya kutumia Kiswahili katika vyombo vyote vya habari kama redio, magazeti, majarida na hata kanda za video kusambaza habari zinazohusiana na maendeleo. Kwa sasa, idhaa za redio ndizo hutumia Kiswahili kwa wingi ilhali runinga zinatumia lugha hii kwa kiasi tu. Lugha ya Kiswahili hajatumika kuandika majarida ya kilimo, afya, au uchumi ilhali Kiingereza ndicho kilichotawala katika uwanja huu. Matokeo ya mwelekeo huu ni kwamba idadi kubwa ya watu wasio na elimu katika sekta zote za maendeleo hawaelewi mambo mengi ambayo yangewafaa kujiendezea kwa vile Kiingereza hakieleweki kwao.

Vilevile, kuna haja ya kutafsiri matokeo ya tafiti mbalimbali zinazofanyika nchini Kenya na kwingineko kwa lugha ya Kiswahili ili maarifa ya tafiti hizo yaweze kuwafikia walio wengi na wanaoelewa Kiswahili. Hili likifanyika, tafsiri hizi zinapaswa kuwekwa katika sehemu maalumu za maktaba za kitaifa na vituo vya kijamii vinavyowahamasisha wananchi kuhusu masuala ya maendeleo. Kwa jinsi hii, maarifa mapya yatawafikia Wakenya wengi. Maarifa tunayoyazungumzia hapa ni pamoja na yale yanayopakuliwa kutohana kwenye tovuti. Katika mustakabali huu, mradi wa kampuni ya *Microsoft* wa kufikisha teknolojia ya mawasiliano, hasa kwa tovuti, sehemu za mashambani hauna budi kuigwa na kuungwa mkono na serikali ya Kenya. Iwapo utafanikiwa,

utawawezesha watu ambao wana elimu kupakua maarifa, hasa maafisa wanaohamasisha maendeleo, na kuyaeneza kwa watu wengine kwa kutumia Kiswahili.

Hata hivyo hakuna utafiti ambao umefanywa kuchunguza uenezaji wa Kiswahili na matumizi yake, hasa katika maeneo ya mashambani. Wataalamu wa lugha ya Kiswahili wana jukumu la kufanya hivi ili kupendekeza hatua za kufanikisha lugha hii.

6.0 Hitimisho

Kwa kuhitimisha mjadala huu tunaweza kusema kwamba Wakenya wanahitaji lugha itakayowawezesha kuelewa na kufanya maamuzi ya masuala ya afya, usafi, kilimo, elimu ya uraia, uchumi, na masuala mengine yote yanayohusu maisha yao ya kawaida. Ili kuongeza uzalishaji mionganoni mwa Wakenya, kuna haja ya kupunguza pengo la kimawasiliano kati ya watafiti, waenezaji wa maarifa (wanasayansi) na wapokeaji wa maarifa na teknolojia inayozalishwa ili kukuza usambazaji wa huduma na kuchochea uzalishaji wa bidhaa za viwandani. Ingawa Kiswahili kinatekeleza majukumu haya yote, pana vikwazo vichache vinavyoikabili lugha hii. Kwanza, ni kuwepo kwa stesheni nyingi za redio zinazotumia lugha za wenyeji kutangazia. Hali hii inaweza kurekeblishwa kisera kupitia ngazi zinazohusika. Jambo lingine ni uhaba wa magazeti ya Kiswahili. Kikwazo hiki kinatokana na ukweli kwamba watu wengi nchini Kenya hawajui kusoma na wanaojua kusoma wana uzembe wa kusoma. Hivyo, inakuwa vigumu makampuni ya uchapishaji kuchapisha magazeti kwa kuwa hayatapata wanunuzi. Hivyo, kuna haja ya kuhakikisha elimu imewafikia wengi kwa kuwa bila elimu usomaji hauwezi kuimarika. Hatimaye, tafiti nyingi za Kiswahili zitasambazwa.

Kupitia mjadala huu ni wazi kuwa Kiswahili ni lugha muhimu sana katika maeneo ya mashambani. Lugha hii ndiyo inayozungumzwa na wengi katika mawasiliano ya kawaida. Hivyo, haina budi kuendelezwa ili iweze kupiga hatua. Kwa mintarafu hii, wataalamu wa nyanja zote kama vile sheria, afya, kilimo, na kadhalika hawana budi kuwa na ujuzi wa Kiswahili ili waweze kuwasiliana na watu wa mashambani kwa urahisi kuhusu masuala ya nyanja zao. Ifahamike kuwa lugha husaidia sana kuudhibiti uhusiano wa kijamii. Lugha ndiyo inayowawezesha watu kuwa na mwingiliano wenye maana na manufaa. Aidha, lugha ni chombo muhimu cha kuhamasisha hisia za uzalendo na umoja wa kitaifa (Buliba, 2001). Lugha ni nyenzo muhimu ya maendeleo na katika kufanikisha mawasiliano ya kutoa mawazo, hisia, maoni pamoja na maarifa ya jamii kwa ujumla.

Marejeo

- Amenya, A. I. (2007). "Kiswahili katika Maendeleo." Makala isiyochapishwa ya Semina ya Idara iliyowasilishwa katika Idara ya Lugha na Isimu: Chuo Kikuu cha Egerton.
- Buliba, A. S. (2001). "Lugha Utamaduni na Jamii katika Maendeleo ya Kitaifa." In *Kiswahili a Tool for Development: The Multidisciplinary Approach*. Naomi L. Shitemi, et al (eds), Eldoret: Moi University (pg. 53– 59).
- Dutcher. (1982). "The use of the First and Second Language in Primary Education: Selected Case Studies." World Bank Staff working Paper No. 504, Washington D C.
- Mohochi, E. S. (2005) *Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu lugha ya Kiswahili na Athari zake katika Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa Kidato cha Nne katika mikoa ya Pwani na Nyanza, Kenya*. Tasnifu ya Uzamivu (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Egerton: Kenya.
- Muhamedin, Q. N. (2001). "Role of Kiswahili in The Promotion and Development of Participatory Extension Services in Kenya." In *Kiswahili a Tool for Development: The Multidisciplinary Approach*. Naomi L. Shitemi, et al (eds) Eldoret: Moi University Press (74– 79).
- Mukuthuria, M. (2009). "Uhakiki wa Mtafaruku wa Istilahi za Kiisimu na Nafasi ya Usanifishaji katika Maendeleo ya Kiswahili." Katika M. M. Mulokozi na G. Mrikaria (Wah.) *Mulika* Na. 28, Uk. 48 -61, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- Mutahi, K. (2001). "Kiswahili as a Tool for Development in Kenya." In *Kiswahili a Tool for Development: The Multidisciplinary Approach*. Naomi L. Shitemi, et al (eds) Eldoret: Moi University Press (8 – 13).
- Nyerere, J. (1967). *Education for Self Reliance*. Dar es Salaam: Government Printers
- Rono, P. K. (2001). "Communication of New Ideas and Innovations: The Role of Language and Change Agents in Rural Development Process." In *Kiswahili a Tool for Development: The Multidisciplinary Approach*. Naomi L. Shitemi, et al (eds) Eldoret: Moi University Press, (133 – 140).
- Severin, W.J. and J.W. (Jr.) Tankard. (1992). *Communication Theories: Original Methods and Uvuse in the Mass media (3rd ed.)*. New York and London: Longman.
- Todaro, M. P. (1994). *Economic Development*. New York: Longman.
- Todaro, M. P. (1980). *Economics for a Developing World*. London: Longman.
- Wiener, N. (1948). *Cybernetics*: Massachusetts Institute of Technology.